



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UFAFANUZI WA BEI ZA MAFUTA
MIKOA YA RUVUMA, MTWARA NA LINDI**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa bei mpya za mafuta zilizoanza kutumika Juni 3, 2020; ambazo zimepungua kwa kiwango kikubwa kwa mafuta yaliyoingilia Bandari ya Dar es Salaam.

Hali ni tofauti kwa mafuta yaliyoingilia Bandari ya Mtwara, ambapo bei zake zimebaki zile za Mei 2020, hivyo kufanya mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi kuwa na bei kubwa kuliko mafuta yaliyoingilia Bandari ya Dar es Salaam.

Hii ni kwa sababu hakukuwa na shehena mpya ya mafuta iliyopokelewa katika Bandari ya Mtwara kwa matumizi ya mwezi Juni, 2020.

Hivyo basi, bei zinatarajiwa kubadilika baada ya kupokea shehena mpya ya mafuta kupitia Bandari ya Mtwara, inayohudumia mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi.

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU

03 Juni, 2020